

Makosa ya Kimofolojia ya Watumiaji wa Kiswahili na Sababu zake: Uchunguzi Kifani wa Watumiaji wa Kiswahili na Kihaya

*Anold Kamugisha*¹
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.3>

Ikisiri

Watumiaji wa lugha ya Kiswahili wanapotumia lugha hiyo vibaya huibua makosa mbalimbali katika vipengele vya kiisimu. Makosa hayo yanaweza kuwa ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisémantiki au kipragmatiki. Makala haya yanachunguza makosa ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili na sababu zake kwa kuhusisha watumiaji wa lugha ya Kiswahili na Kihaya. Data za msingi zilikusanywa uwandani kwa kutumia mbinu ya majadiliano katika vikundi lengwa na mbinu ya insha. Uchambuzi wa data za utafiti uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari iliyoasisiwa na Corder (1967). Imebainika kuwa kuna makosa anuwai ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Makosa hayo ni pamoja na kuongeza viambishi visivyohitajika kwenye neno, uchanganyaji msimbo, kutumia ngeli za nomino zisizo sahihi, kuhawilisha maumbo ya maneno ya Kiingereza katika Kiswahili na matumizi ya maumbo ya lughatandawazi. Pia, imebainika kwamba makosa hayo husababishwa na wazungumzaji kutojua vyema lugha ya Kiswahili, athari ya lugha ya Kihaya katika Kiswahili, tafsiri sisizi na ufanano wa kiumbo wa maneno ya Kiswahili na Kihaya. Aidha, makala haya yamebaini kwamba makosa hayo huleta athari mbalimbali kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili kama vile kushindwa kumudu ruwaza za lugha hiyo. Hivyo, watumiaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine, hawana budi kuacha ujumuishaji wa kuhawilisha maumbo yasiyo sahihi. Badala yake, wajifunze ngeli za nomino ili waweze kutumia maumbo sahihi ambayo yanakubalika katika lugha ya Kiswahili kwa azma kuzingatia sarufi ya lugha ya Kiswahili, utamaduni wa jamii na kuepuka kubananga lugha ya Kiswahili.

1.0 Utangulizi

Watumiaji wa lugha anuwai za Kibantu hufanya makosa mbalimbali wanapotumia lugha ya Kiswahili. Hali hii pia inajitokeza katika jamii ya Wahaya wanapotumia Kiswahili katika mawasiliano yao kwa njia ya mazungumzo na maandishi. Tafiti tangulizi zinazohusu makosa ya kiisimu zimechunguza makosa hayo ya kiisimu yanayofanywa na wanafunzi na waandishi wa vyombo vya habari hususani magazeti katika viwango anuwai vya isimu. Hata hivyo, tafiti zilizochunguza makosa ya kimofolojia zinakanganya makosa hayo na makosa ya viwango vingine

¹ Barua pepe: anoldkamugisha8@gmail.com

vya isimu. Kadhalika, watumiaji wa Kiswahili kwa ujumla ambao si wanafunzi wala waandishi wa magazeti, hufanya makosa ya kiisimu yakiwamo ya kimofolojia. Aidha, makosa yanayofanywa na jamiilugha moja katika matumizi ya Kiswahili yanaweza kufanana au kutofautiana na makosa yanayofanywa na jamiilugha nyingine. Hivyo basi, makala haya yamechunguza makosa mbalimbali ya kimofolojia yanayofanywa na Wahaya wanapotumia Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku, na kuangalia maumbo ya maneno ya Kiswahili yanayotumiwa na Wahaya na ukubalifu wa maumbo hayo katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Makosa katika lugha ni utumizi usio sahihi wa kanuni za lugha unaotokana na kutozingatiwa kwa sarufi ya lugha, utamaduni wa jamii na mikakati mbalimbali ya lugha husika ambao hufanywa na mtumiaji lugha ambaye hajaelewa vizuri sheria za lugha lengwa (Larsen, 1992; Jabeen na wenzake, 2015). Makosa yanayofanywa na mtumiaji lugha yanaweza kuwa katika kiwango cha fonimu, mofimu, neno au sentensi katika lugha mahususi. Katika lugha, makosa ni matokeo ya mtumiaji lugha kushindwa kutumia lugha kwa ufasaha.

Makosa ya kimofolojia ni ukiukwaji wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofu mbalimbali katika kuunda maneno yenye maana sahihi katika lugha (Mghase, 2011). Makosa hayo yanahusisha vipengele anuwai vya kimofolojia kama vile mofu, mofimu na msamiati ambavyo vimeshughulikiwa katika makala haya. Aidha, makosa ya kimofolojia yanaweza kudhihirika kwa njia ya mazungumzo na maandishi kutokana na ukiukwaji wa taratibu za uundaji na utumiaji wa maneno ya lugha.

Obara (2014) alichunguza makosa katika kiwango cha mofolojia yanayofanywa na wanafunzi wanaozungumza lugha ya Ekegusii Magharibi mwa Kenya. Katika utafiti wake anabainisha makosa ya kimofolojia kuwa ni pamoja na uchopekaji wa irabu /u/, udondoshaji wa sauti /h/, uyeyushaji na muundo wa silabi usiofaa kwa kutoa mifano ya tungo zilizooneshwa katika Data Na. 1 ifuatayo:

Data Na. 1

- (i) a.* Hapo nilichelewa *kuamuka*----
b. Hapo nilichelewa *kuamka*----
- (ii) a.* *Niliamuka asubui* na mapema----
b. *Niliamka asubuhi* na mapema----
- (iii) a.* ---baada ya *kimia* cha dakika tatu----
b.----baada ya *kimya* cha dakika tatu----

Chanzo: Obara (2014: 43-46)

Katika Data Na. 1 (i-iii), tungo zenye alama ya nyota (*) zinaonesha makosa mbalimbali ambapo tungo namba (i) inaonesha uchopekaji wa irabu /u/ katika neno *kuamuka* badala ya 'kuamka'. Tungo namba (ii) inaonesha uchopekaji wa

irabu /u/ katika neno *niliamuka* badala ya 'niliamka' na udondoshaji wa konsonanti /h/ katika neno *asubui* badala ya 'asubuhi'. Kadhalika, tungo namba (iii) inaonesha ubadalalishaji wa sauti, ambapo kiyeyusho /y/ katika neno 'kimya' kimebadalalishwa na irabu /i/ katika neno *kimia* badala ya kuwa neno 'kimya'. Hata hivyo, makosa hayo siyo ya kimofolojia kama asemavyo Obara (2014), bali ni makosa ya kifonolojia kwa sababu yanadokeza vipengele vya fonolojia katika Kiswahili.

Pia, Mutungu (2001), Kisakwah (2014) na Nyagah (2016) walichunguza makosa mbalimbali ya kiisimu katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Wataalamu hao wanabainisha makosa yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuwa ni pamoja na tafsiri isiyofaa; uchopekaji wa irabu; unazalishaji wa fonimu; udondoshaji wa sauti; ukiushi wa viambishi vipatanishi vya ngeli; na matumizi mabaya ya vivumishi, vihusishi, viunganishi na virejeshi. Makosa yaliyobainishwa na wataalamu hao yamejikita zaidi katika kiwango cha fonolojia na sintaksia.

Halikadhalika, Kemunto na wenzake (2017) wameangalia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Katika kuangazia makosa hayo, wataalamu hao wanabainisha makosa ya kisemantiki kuwa ni pamoja na matumizi ya msamiati usiofaa, kuacha sauti katika neno, matumizi ya lugha ya ushairi, ufafanuzi uliokithiri, mrundikano wa maneno katika sentensi, matumizi ya msimbo wa sheng, kutumia sauti isiyofaa katika neno na ukiukwaji wa sheria za lugha lengwa. Hivyo, ili kuepukana na makosa hayo, watumiaji wa lugha ya Kiswahili hawana budi kufanya mazoezi ya kutosha katika uandishi na uzungumzaji wa Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya makosa yaliyobainishwa kama vile kuacha sauti katika neno si ya kisemantiki, bali ni ya kifonolojia.

Vilevile, Joster (2018) alichunguza makosa ya kiuhariri katika vitabu vya kiada vya Kiswahili nchini Tanzania. Utafiti wake ulibainisha makosa hayo kuwa ni pamoja na makosa ya matumizi ya herufi kubwa, uandikaji wa vichwa vya habari na matumizi ya finyazo na vifupisho. Makosa ya matumizi ya herufi kubwa kama vile makosa ya majina mahususi ya mahali, majina ya asasi mbalimbali na majina ya sikukuu na matukio ya kihistoria yanajikita katika kiwango cha mofolojia, kwa sababu yanaangalia usahihi wa umbo la neno. Hata hivyo, data ya utafiti wa Joster ilijikita katika maandishi tu, tofauti na utafiti huu ambao ulijikita katika data ya maandishi na mazungumzo. Kadhalika, Joster alishughulikia makosa ya kiuhariri, ilhali utafiti huu umeangalia makosa ya kimofolojia.

Naye Mpemba (2018) alichunguza matatizo ya uandishi katika Kiswahili kwa kuangalia maana, chanzo na ufumbuzi. Utafiti wake ulibainisha matatizo yanayohusu mbinu na taratibu za uandishi kuwa ni pamoja na matatizo ya kiuafikishi, unafasishaji na utumizi wa herufi kubwa. Aidha, Mpemba (*khj*)

alibainisha matatizo ya kawaida ndani ya lugha kwa kuonesha matatizo ya kifonolojia na kisintaksia pasi kugusia matatizo ya kimofolojia.

Kwa upande mwingine, Rapando (2005) na Hepkwony (2011) wanaeleza sababu mbalimbali za makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika Kiswahili kuwa ni pamoja na ujumuishaji wa kanuni za lugha ya kwanza (L1 kuanzia sasa) katika kutumia Kiswahili, kutojua upatanisho wa kisarufi na utofauti wa miundo ya sentensi za lugha moja na nyingine. Wataalamu hawa walichunguza sababu hizo katika kiwango cha mofosintaksia kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwa kujikita zaidi katika data ya maandishi bila kugusia data ya mazungumzo na watumiaji wengine wa lugha ambao si wanafunzi. Pia, Mghase (2011) anaelezea sababu za makosa ya kiisimu katika uandishi wa magazeti. Sababu hizo ni kutokuelewa maana za maneno yaliyotumika katika uandishi, athari ya lugha ya mazungumzo katika maandishi na mazoea mabaya ya matumizi ya maneno mbalimbali. Hata hivyo, sababu zilizobainishwa na Mghase zimejiegemeza kwa maandishi wa habari za magazeti.

Kwa ujumla, maandiko mbalimbali yaliyopitiwa yameangazia makosa yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali vya isimu. Hata hivyo, makosa ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa Kiswahili yameangaziwa kwa uvulivuli. Hivyo, makala haya yamechunguza makosa ya kimofolojia na sababu zinazokilia makosa hayo katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano.

2.0 Mbinu za Utafiti na Nadharia

Data za msingi za utafiti uliozaa makala haya zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi lengwa na mbinu ya insha. Mtafiti alitumia mbinu hizo kukusanya data zinazohusu makosa ya kimofolojia yanayofanywa na Wahaya wanapotumia Kiswahili. Mbinu ya majadiliano ilimsaidia mtafiti kufafanua sababu za makosa hayo ili kupata data zinazohusu sababu zinazokilia makosa ya kimofolojia. Kadhalika, mbinu ya insha ilimsaidia mtafiti kupata data ya maandishi ili kubaini makosa mbalimbali yanayojitokeza kwenye maandishi. Mbinu hizo zilisaidia kuchangamana na watoataarifa na hivyo kupata data halisi kuhusu utumiaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wahaya. Kwa hiyo, mtafiti alitumia mbinu hizo ili kupata data ya mazungumzo na maandishi.

Mbinu ya majadiliano ilitumika kukusanya data kutoka kwa watoataarifa sabini na wawili (72) ambao ni watoto, vijana na watu wazima, ambapo kila kundi lilikuwa na watoataarifa ishirini na wanne (24). Watoataarifa hao walipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi, usampulishaji nasibu sahili na usampulishaji tajwa. Mtafiti alijadiliana na watoataarifa hao kuhusu shughuli mbalimbali wanazozifanya kila siku kama vile michezo, mapenzi, ajira, changamoto za kimaisha, masuala yanayohusu utamaduni wa jamii ya Wahaya,

hali ya maisha, nafasi ya mwanamke, umuhimu wa elimu katika jamii na mazingira. Kadhalika, mbinu ya insha ilitumika kukusanya data kutoka watoto na vijana, ambapo waliandika insha kwa dakika zisizozidi kumi kuhusu mada mbalimbali za masuala ya kijamii. Aidha, watu wazima wengi hawakutaka kuandika, bali walishiriki majadiliano kwa muda wa dakika ishirini hadi thelathini.

Data za makosa haya zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui kwa kusimba na kusimbua data zilizokusanywa. Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti alichunguza makosa ya kimofolojia na kuyawekea alama. Makosa yaliyofanana yaliwekwa katika kundi moja ili kubaini kosa husika. Halikadhalika, baada ya kubaini kosa husika, mtafiti alitumia maelezo kufafanua makosa ya kimofolojia yaliyojitokeza pamoja na sababu za makosa hayo. Mbinu hii ilikuwa mwafaka zaidi kwa sababu ilimsaidia mtafiti kufafanua data kwa kufuata utaratibu maalumu wa kusimba na kusimbua data zilizokusanywa.

Aidha, makala haya yameongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari (kuanzia sasa NUD). NUD iliasisiwa na Corder mwaka 1967. NUD imejiegemeza kuchunguza makosa ya lugha za Kibantu na sababu za makosa hayo kama vile mwingiliano wa L1 na lugha ya pili (kuanzia sasa L2), ujumuishaji, mtazamo, kipaji na motisha. Mhimili mkuu wa NUD ni kwamba makosa mengi ya watumiaji wa L2 hutokana na watumiaji wenyewe kukosea kanuni za L2 katika mawasiliano. Kwa upande mwingine, Corder (1967) anasema kwamba licha ya mwingiliano wa L1, kuna sababu nyingine za ufanyaji wa makosa kwa watumiaji lugha. Anathibitisha madai haya kutokana na utafiti wake ambapo alibaini kwamba 3% ya makosa ya watumiaji wa lugha hutokana na mwingiliano wa L1 na L2 na 85% hutokana na makosa yanayojitokeza katika mchakato wa ujifunzaji na utumiaji wa lugha husika.

NUD imejiegemeza katika mhimili mkuu wa kuangalia makosa yanayotokana na kanuni za L2. Kutokana na mhimili huo, NUD inahusisha misingi mikuu mitano katika kuchunguza makosa. Misingi hiyo ni: kukusanya sampuli ya watumiaji lugha, kubainisha dosari, kufafanua dosari, kutafuta chanzo cha dosari na kutathmini dosari (Corder, 1967). Makala haya yamezingatia misingi yote mitano ya NUD ili kubaini makosa na sababu za makosa ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu, mtafiti alikusanya sampuli ya watumiaji lugha ya Kiswahili, akakusanya data kisha akabaini makosa katika data zilizokusanywa, akafafanua makosa na vyanzo vyake, halafu mwishoni akatathmini makosa hayo katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Corder (1967) anafafanua kwamba makosa hutokana na vyanzo vikuu viwili. Mosi, makosa yanayotokana na mwingiliano wa L1 na L2. Pili, makosa yanayotokana na mtumiaji lugha mwenyewe kutojua kanuni za lugha anayoitumia. Katika uchambuzi wa data, nadharia hii ilikuwa mwafaka kwani vyanzo hivyo vimebainishwa kutokana na data iliyokusanywa. Hata hivyo, utafiti

huu umebaini sababu nyingine ambazo hazikufafanuliwa na Corder. Kwa ujumla, NUD ilikidhi kuchambua makosa na sababu za makosa katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu makosa katika lugha husababishwa na masuala kadhaa, ikiwamo mchakato wa utumiaji wa lugha husika.

3.0 Makosa ya Kimofolojia Yanayofanywa na Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii imechambua makosa mbalimbali ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili kama ilivyobainishwa na utafiti huu.

3.2 Kuongeza Viambishi Visivyohitajika kwenye Neno

Uongezaji wa viambishi ni kitendo cha kuweka vipashio katika neno fulani na hivyo kulifanya neno husika kuwa na viambishi ama vinavyotakiwa au visivyotakiwa na pengine kuathiri maana ya neno hilo. Uongezaji wa viambishi unaweza kuwa mwanzoni au mwishoni mwa neno. Matokeo ya utafiti huu yamebaini uongezaji wa viambishi visivyohitajika kwenye maneno mbalimbali ya Kiswahili. Viambishi vinavyoongezwa katika neno ni {*po*, *mo* na *ko*} ambavyo havitakiwi kuwapo katika maumbo ya Kiswahili. Baadhi ya viambishi hivyo vinabainishwa katika dondoo la Data Na. 2.

Data Na. 2

Hadithi kuhusu mbwa mwitu na swala

Siku moja nilikwato ninachunga ng'ombe mala moja nikaanguka kulia kwangu nikaamwona mbwamwitu aki mfukwa swala ng'ombe wakoogopa na kukimbia aygo mbwamwitu akaanza kumfukwa ng'ombe namini ndipo nilikimbia nikaendelea kumfukwa mbwa mwitu alipona niki mfukwa ndipo alitabata na kuana kunitujiza mimi namini nilijikwa kisabuni ni komba aliponitabata na mimi nika mkaribia nilimtu pia m tuki kikuani na ng'ombe wakatoka na kuelekea nilipo mara moja mbwa nilipomshoma mkuki alianguka vibaga na kutas pumuzi ya mwisho nikawapeleka ng'ombe ng umboni ni kawasimulia nilivyo mchamako mkuki si mba akaanguka nyumboni wabaisi fiapo na mimi ndipo nitana kuwa mimi ni mwindaaji bore na jasi nika tokako kwa yajasi wangu.

HADITHI KUHUSU SUNGURA NA FISI

Hapo zamani za kale palikuwepo sungura na fisi.
Siku moja Sungura alikuwa bize na kupika chakula.
Sasa fisi alikuwa ameabikwa kwenye arusi ya Sungura.
Mke wake fisi na watoto wake na Anko walikuja wakaruka Sungura anapita mchele akawambia karikuni Ingizimo ndani ni wotelee Kinywaji walipo fika ndani wakafeti dini ya mitetia Anki akosema mba na haliyi Sungura na hawituleki Kinywaji. Sungura akosema niko bize Msiisumbue nita wafukwa mimi si kuwarika majiteta kulona kunyewa vitu vya watu. Fisi akosema wasamehe hawakujua wanacho kifanya akosema Wewe fisi wetkamo chakula kwenye bahani wote wa Kimalizi waondoke mara moja.
Hadithi yangu inaishia hapo.

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Makosa yaliyojitokeza katika Data Na. 2 yanabainishwa katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Mifano ya Makosa ya Kuongeza Viambishi Visivyohitajika kwenye Neno

Na.	Kosa	Maneno Sahihi
i.	<i>alitokako</i>	alitoka huko
ii.	<i>ameendako</i>	ameenda huko
iii.	<i>nilikuwako</i>	nilikuwa huko
iv.	<i>alikuwamo</i>	alikuwa humu
v.	<i>wekamo</i>	weka humu
vi.	<i>aliendamo</i>	alienda humo
vii.	<i>nitakujapo</i>	nitakuja hapo
viii.	<i>sijajapo</i>	sijaja hapo
ix.	<i>waendapo</i>	unaenda hapo

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Mifano iliyotolewa katika Jedwali Na. 1 (i-ix) inaonesha uongezaji wa viambishi {*po*, *mo* na *ko*} mwishoni mwa neno. Hali hiyo ya uongezaji wa viambishi inafanya neno husika kutokeza dhana ya umahali katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya watumiaji wa Kiswahili hususani Wahaya, wanapotumia maneno hayo, hawakusudii kuonesha mahali, bali huyatumia kimazoea na wakati mwingine bila kujua usahihi wake. Hali hii husababishwa na athari ya lugha mama na kutojua vema lugha ya Kiswahili. Aidha, uongezaji wa viambishi hivyo hutokana na athari za lugha ya Kihaya katika Kiswahili. Mathalani, katika lugha ya Kihaya kuna viambishi {*yo* na *mu*} ambavyo hujitokeza mwishoni mwa baadhi ya maneno, mfano: *tindiyo*-sipo, *nagyayo*-nimeenda, *tekayo*-weka, *natamu*-nimeweka. Hivyo, baadhi ya maneno yanayoishia na kiambishi {*yo*} na {*mu*} katika lugha ya Kihaya huhawilishwa kuwa kiambishi {*po*} na {*mo*} mtawalia katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, viambishi {*po*, *ko* na *mo*} hubeba dhima ya kuwa vibainishi vioneshi vya mahali katika lugha ya Kiswahili (Champungwa, 2019). Viambishi vioneshi vya mahali hupachikwa mwishoni mwa kitenzi katika mazingira ambayo kitenzi huwa na kiambishi awali cha nafsi au kipatanishi + shina + {*po/cho/mo/ko*}. Hata hivyo, vitenzi vilivyopo katika Jedwali Na. 1 (i-ix) haviruhusu kupachikwa viambishi vioneshi vya mahali mwishoni pasipo kudondosha njeo. Hivyo, ili viambishi hivyo vikubalike kupachikwa mwishoni mwa kitenzi, ni sharti kudondosha njeo katika neno husika. Hali hii husababishwa na mwingiliano wa matumizi ya maneno ya Kihaya na Kiswahili kama asemavyo Corder (1967) katika NUD kwamba 3% ya makosa ya watumiaji wa lugha hutokana na mwingiliano wa L1 na L2 na 85% hujitokeza katika mchakato wa ujifunzaji na utumiaji wa lugha husika.

3.2 Kuhawilisha Maumbo ya Maneno ya Kiingereza katika Kiswahili

Dhana ya uhawilishaji hurejelea kuhamisha maarifa, ujumbe, mawazo au maneno kutoka lugha moja kwenda nyingine kwa njia ya maandishi au mazungumzo.

Uhawilishaji unatokana na hali ya kaida za lugha moja kutumiwa katika lugha nyingine kimatamshi, kimaumbo na kimuundo. Uhawilishaji lugha hujitokeza katika vipengele vyote vya isimu, yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Data iliyokusanywa kutoka kwa vijana na kudondolewa katika majadiliano mbalimbali ya vikundi lengwa, inadhihirisha makosa ya uhawilishaji wa maumbo ya maneno ya lugha ya Kiingereza katika utumiaji wa Kiswahili. Makosa ya namna hiyo yanabainishwa katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Mifano ya Makosa ya Kuhawilisha Maumbo ya Maneno ya Lugha ya Kiingereza katika Kiswahili

Na.	Neno Asilia	Neno Lililohawilishwa	Neno Sahihi
i.	<i>mother</i>	<i>maza</i>	mama
ii.	<i>uncle</i>	<i>anko</i>	mjomba
iii.	<i>aunt</i>	<i>anti</i>	shangazi
iv.	<i>home</i>	<i>homu</i>	nyumbani
v.	<i>teacher</i>	<i>ticha</i>	mwalimu
vi.	<i>busy</i>	<i>bize</i>	tingwa

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data zilizopo katika Jedwali Na. 2 zinaonesha maneno mbalimbali ambayo yamehawilishwa kutoka lugha ya Kiingereza na kutumiwa katika lugha ya Kiswahili. Uhawilishaji huo unatokana na kutumia maneno kwa namna ambavyo yanatamkika katika lugha ya Kiingereza. Hali hii inatokana na mwingiliano wa jamiilugha kati ya wasomi na ambao hawajasoma pamoja na watu wanaoishi mijini na wale wa vijijini, suala ambalo husababisha kutumia maneno ya Kiswahili kimazoea pasi kuzingatia usahihi wa maneno hayo. Halikadhalika, data za utafiti huu zimeonesha kwamba maneno hayo huhawilishwa kimakosa kwa njia ya mazungumzo kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili na hivyo kuzua mazoea mabaya ya matumizi ya maneno mbalimbali. Hoja hii inashadidiwa na NUD inayodai kwamba baadhi ya makosa yanatokana na mtumiaji lugha mwenyewe kutojua kanuni za lugha anayoitumia (Corder, 1967).

Hivyo, makosa ya kuhawilisha maumbo ya maneno kutoka lugha za kigeni na kutumiwa katika lugha ya Kiswahili husababisha kupata maumbo ya maneno yasiyo sahihi katika lugha ya Kiswahili. Hoja hii inashadidiwa na maelezo ya Hussein (2016) anayedai kwamba baadhi ya maneno ya Kiarabu yameingizwa kwa makosa katika Kiswahili na kupewa maana nyingine ambazo ni tofauti na maana ya asili. Hata hivyo, data ya utafiti huu inaonesha kwamba maneno yanayohawilishwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili yanapewa maana ileile kama ilivyo katika lugha asili, japo maumbo ya maneno hayo si sahihi katika lugha ya Kiswahili. Kwa msingi huo, tunaweza kusema kwamba maumbo ya maneno yaliyobainishwa katika Jedwali Na. 2 si sahihi kwa sababu

hayakubaliki na hayajasanifishwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, kuna baadhi ya maneno kama vile *mota*, *data*, *mita*, *hita na friji* ambayo yamehawilishwa kutoka lugha ya Kiingereza na kutumiwa katika lugha ya Kiswahili. Maneno hayo yanakubalika katika Kiswahili sanifu, japo yana visawe vyake. Hata hivyo, maneno yaliyopo katika Jedwali Na. 2 si kubalifu katika lugha ya Kiswahili sanifu na hayana visawe katika lugha hiyo.

3.3 Uchanganyaji Msimbo

Msimbo ni mfumo wa ishara zinazotumika katika mawasiliano au shughuli fulani maalumu. Uchanganyaji msimbo ni utumizi wa lugha mbili au zaidi katika semo au kirai kimoja ambao unaweza kujitokeza katika mofimu, neno, kirai, kishazi au sentensi za lugha moja au lugha zaidi ya moja (Muysken, 2000). Uchanganyaji msimbo husababishwa na hali ya kuingiliana na kuathiriana kwa lugha katika viwango mbalimbali. Data ya utafiti huu inadhihirisha uchanganyaji msimbo katika kiwango cha neno, ambapo athari ya uchanganyaji msimbo ni kuunda neno lisilo sahihi katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya makosa hayo yanabainishwa katika dondoo la Data Na. 3.

Data Na. 3.

Hali' ya Maisha

*Maisha ya Sasa ~~zametaki~~ Sana esa upatkausi
 wa now ni ngumu. Aila hamu na Washava
 ngumu kwani hamu mzunguko. Hali' hi' imeong-
 eza wizi na utepeli.*

*Kiukweli maisha ya Sasa yanahitaji ubunifu
 na urunwili wa hali' ya juu. Kwa hali' hi'
 umaskini hauwezi ~~tekwa~~ maana hata
 kupata mazi ni shida.*

Michezo

Michezo ni sekte muhimu sana kwa ajira yetu na umuhimu wa taifa lolote. Ukicheki umuhimu wa michezo kwa mtazamo pana utarona kwamba ni muhimu katika maisha yetu.

Michezo imekuwa chanzo cha ajira na kupata hela za kigeni. Mfano wachezaji wa nje kama Jamata na Msuva hukipwa kwa dola. Wachezaji hukipia kodi ambapo serikoni upata mapato mengi.

Michezo inayolingia hela ni nyingi, ila kubeti ni michezo ambao upendwa na vijana wengi. Michezo wa kubeti unadewa na watu wote hasa watoto na vijana. Michezo mingine kama football ina mas kubiki wengi. Kichekeli kupitia michezo tunaenjoi sura

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Makosa yaliyojitokeza katika Data Na. 3 na makosa mengine yaliyojitokeza kwa njia ya majadiliano ya vikundi lengwa yanabainishwa katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3: Mifano ya Makosa ya Uchanganyaji Msimbo

Na.	Kiswahili	Kiingereza	Msimbo (Kosa)	Neno/Maneno Sahihi ya Kiswahili
i.	ku	bet	kubeti	kubashiri
ii.	nitaku	support	nitakusapoti	nitakuunga mkono
iii.	nitawa	call	nitawakolo	nitawapigia simu/kuwaita
iv.	tuta	meet	tutamiti	tutakutana
v.	tuna	enjoy	tunaenjoi	tunafurahia
vi.	uki	check	ukicheki*	ukiangalia
vii.	utu	follow	utufolo	utufuate
viii.	yame	tight	yametaiti	yamebana

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Maneno yaliyobainishwa katika Jedwali Na. 3 yanaonesha uchanganyaji msimbo katika kiwango cha neno, hivyo, kuibua maneno yasiyokubalika katika lugha ya Kiswahili isipokuwa Na. vi. Licha ya kwamba neno cheki limeundwa kutokana na uchanganyaji msimbo, lakini neno hilo limerasimishwa katika kamusi na kumaanisha tazama kwa madhumuni ya kusahihisha au kusadikisha (TUKI, 2019). Ijapokuwa maana inayorejelewa katika makala haya ni angalia na ile ya kikamusi ni tazama; maneno haya yanaweza kurejelewa kama visawe, lakini hutofautiana kimuktadha. Aidha, maneno mengine yaliyopo katika Jedwali Na. 3 yanaonesha mwambatano wa neno moja ambalo limetokana na mofu za lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mofu zinazowakilisha mofimu za maneno hazikubaliki na haziendani na sarufi ya lugha ya Kiswahili (Kiparsky, 1982). Kwa hiyo, mwambatano wowote wa maneno lazima utoe muundo sahihi wa neno linalokubalika katika lugha ya Kiswahili. Vilevile, maneno ya Kiswahili sanifu hayakubali kuchanganya mofu za lugha mbili tofauti ili kuunda neno moja katika lugha ya Kiswahili.

Hivyo, neno *bet, support, call, meet, enjoy, check, follow* na *tight* ni msamiati ambao ni vitenzi vya lugha ya Kiingereza. Kadhalika, maumbo {*ku, nitaku, nitawa, tuta, tuna, utu na yame*} ni ya lugha ya Kiswahili na hupata maana yanapopachikwa katika neno husika. Kwa hiyo, mofu hizo zinapaswa kuambatana na vitenzi sahihi vya Kiswahili ili kuibua maneno yanayokubalika katika lugha ya Kiswahili. Hali hii hutokana na kuiga mitindo mbalimbali ya utumizi wa lugha na kukosa msamiati sahihi wa lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, watumiaji hao huchanganya msimbo ili kufidia upungufu wa msamiati walionao katika lugha ya Kiswahili na wakati mwingine maneno hayo hutumiwa kimazoea. Hali hii husababishwa na watumiaji wenyewe kukosea kanuni za L2 katika mawasiliano kama unavyodai mhimili mkuu wa NUD (Corder, 1967). Aidha, kwa kuwa maneno yenye misimbo yaliyobainishwa katika Jedwali Na. 3 yanatumiwa sana na watumiaji wengi wa Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku, yanaweza kusanifishwa na kuingizwa katika kamusi kama vidahizo ili kupewa taarifa zote za kileksikografia. Mathalani, neno *cheki* (Jedwali Na. 3, Data Na. vi) ambalo linatumiwa katika Kiswahili sanifu kwa maana ya 'kutazama kwa madhumuni maalumu (kagua)', linaweza kuongezewa kisawe cha angalia kama ambavyo limerejelewa kwa maana hiyohiyo katika data ya utafiti huu.

3.4 Makosa katika Matumizi ya Ngeli za Nomino

Ngeli za nomino ni upangaji wa nomino za lugha katika makundi yaliyoshikamana na kufungamana kutokana na vigezo maalumu. Uainishaji wa ngeli za nomino unaweza kufanywa kwa kuzingatia vigezo vya aina tatu: kigezo cha kisintaksia ambacho huzingatia upatanisho wa kisarufi unaofanana; kigezo cha kimofolojia ambacho huzingatia viambishi vya umoja na wingi, na kigezo cha kisemantiki ambacho huzingatia kiambishi cha nomino na maana (Mugaya, 2018). Data za

utafiti huu zilizodondolewa katika majadiliano mbalimbali ya vijana na watu wazima zinadhihirisha makosa ya kutumia ngeli za nomino kwa kigezo cha kimofolojia ambayo yamebainishwa katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Mifano ya Makosa katika Matumizi ya Ngeli za Nomino

Na.	Kosa	Neno Sahihi
i.	<i>mashule</i>	shule
ii.	<i>manyumba</i>	nyumba
iii.	<i>masaa</i>	saa
iv.	<i>mataa</i>	taa
v.	<i>madawa</i>	dawa

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Katika Jedwali Na. 4 tunabaini makosa ya kutumia ngeli za nomino katika uundaji wa maneno ya Kiswahili. Kimofolojia, ngeli za nomino hutambulisha mofu ya umoja na wingi wa nomino husika. Pia, hueleza kama nomino ina maumbo tofauti ya umoja na wingi au umbo moja katika hali zote za umoja na wingi (Kihore na wenzake, 2007). Nomino *shule*, *nyumba*, *saa*, *taa* na *dawa* zipo katika ngeli ya tano. Sifa kuu ya nomino zote zinazolingia katika ngeli hii huwa na umbo la umoja na wingi linalofanana ambalo ni mofu kapa {Ø}. Hivyo, katika uainishaji wa ngeli za nomino, si nomino zote za Kiswahili huchukua mofu ya wingi. Kwa mantiki hiyo, mofu {**ma**} ikiwekwa katika nomino za ngeli ya tano kumaanisha wingi wa nomino husika huibua makosa katika lugha ya Kiswahili. Aidha, licha ya kwamba mofu za maneno hayo zimepangwa kwa usahihi, lakini maneno hayo hayakubaliki katika lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kutozingatia ngeli za nomino. Hivyo basi, matumizi ya maneno hayo hayakubaliki katika lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kutokuwa sahihi.

Aidha, kwa mujibu wa Kihore na wenzake (2007), nomino za Kiswahili ambazo huchukua mofu {**ma**} ya wingi zipo ngeli ya tatu na ya saba ambazo ni **JI – MA** (**ji**cho – **ma**cho), **U – MA** (**u**gonjwa – **ma**gonjwa) na **Ø – MA** (Ødebe – **ma**debe). Nomino nyingine katika Kiswahili huwa na mofu tofauti za wingi na nyingine huwa na mofu kapa. Kadhalika, Leonard (2008) anasema kuwa nomino za Kihaya ambazo huchukua mofu {**ma**} ya wingi zipo ngeli ya sita ambayo ni **I – MA** (**i**huli/yai – **ma**huli/mayai). Hivyo, uwekaji wa mofu {**ma**} katika nomino za Kiswahili kunazifanya nomino hizo kuhamia ama ngeli ya tatu au ya saba ambazo huwa na mofu {**ji**}, {**u**} na {Ø} katika umoja na mofu {**ma**} katika wingi; kwa mfano, *jiwe-mawe*, *ugonjwa-magonjwa*, *kasha-makasha*. Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kwamba makosa ya kutumia ngeli za nomino yanaweza kusababishwa na ujumuishaji kwa sababu Wahaya wanapotumia Kiswahili hukosea kanuni za lugha hiyo katika mawasiliano. Madai haya yanaungwa mkono na NUD inayodai kwamba 85% ya makosa hujitokeza katika mchakato wa utumiaji wa lugha husika

(Corder, 1967). Licha ya kwamba makosa yaliyopo katika Jedwali Na. 4 yamebainika katika jamii ya Wahaya, lakini mtafiti amebaini kwamba makosa ya namna hiyo yanajitokeza kwa watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili hata wale ambao ni wasomi.

3.5 Matumizi ya Maumbo ya Lughatandawazi

Lughatandawazi ni ile inayotumiwa mitandaoni wakati wa kuandika maneno mbalimbali. Lugha hiyo huwa na mchanganyiko wa maneno, namba na hata kuchanganya lugha zaidi ya moja na hivyo kuunda lugha tofauti na iliyozeleka katika jamii. Sifa kuu ya lugha hii ni ufupishaji ambao hupatikana kwa njia ya kudondosha baadhi ya sauti, silabi na kuwapo kwa matumizi ya namba (Mutembei, 2011). Data zinazohusiana na hoja hii zilizokusanywa kwa njia ya insha kutoka kwa vijana zinadhihirisha matumizi ya lughatandawazi kama ilivyobainishwa katika dondoo la Data Na. 4.

Data Na. 4

Mpira wa Miguu

Mpira wa miguu ni mchezo unachopenda
na waz wengi. Wachezaji wanacheza mpira wa
miguu kupata heri nyingi.

Hapa kwez mpira unachezwa jioni kila
siku. Waz wengi zinakusanyika kwa pai
kuchuki mechi. Binafsi Ezi kukosa hapa
uwajani kwez ninapenda sana kuchuki mechi.

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Katika Data Na. 4, maneno yaliyopigiwa mistari yanaonesha utumiaji na uchanganyaji wa namba na maneno, ambayo ndiyo matumizi ya lughatandawazi. Makosa hayo yaliyobainishwa katika Data Na. 4 na makosa mengine yaliyojitokeza katika insha nyingine zilizoandikwa na vijana yamechambuliwa na kubainishwa katika Jedwali Na. 5 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 5: Mifano ya Makosa ya Kutumia Maumbo ya Lughatandawazi

Na.	Kosa	Neno Sahihi
i.	<i>kwa7bu</i>	kwa sababu
ii.	<i>kwe2</i>	kwetu
iii.	<i>wa2</i>	watu
iv.	<i>wenze2</i>	wenzetu
v.	<i>pa1</i>	pamoja
vi.	<i>2kienda</i>	tukienda
vii.	<i>2nakusanyika</i>	tunakusanyika
viii.	<i>6kosa</i>	sitakosa

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Katika Jedwali Na. 5 tunabaini maumbo ya lughatandawazi ambayo yameandikwa kwa muundo wa kuchanganya namba na silabi. Mithalani, neno *kwa7bu* lina muundo wa silabi+namba+silabi; neno *kwe2* lina muundo wa silabi+namba, vivyo hivyo na maneno mengine kama yalivyobainishwa katika Jedwali Na. 5. Utumiaji na uchanganyaji wa namba na maneno ni jambo ambalo linazua matumizi ya lughatandawazi katika maumbo ya maneno ya Kiswahili, ambapo muundo wa namna hiyo haukubaliki katika kuunda maneno ya lugha ya Kiswahili.

Licha ya Mutembe (2011) na Mohammed (2013) kueleza kuwa maumbo ya lughatandawazi hutumiwa katika mitandao ya kijamii na simu za kiganjani, makala haya yamebaini kwamba maumbo hayo hutumiwa katika maandishi mengine yasiyo ya mitandao ya kijamii, kama ilivyobainika katika insha zilizoandikwa na watoatarifa vijana. Vilevile, makala haya yamebaini kwamba aghalabu matumizi ya maumbo ya lughatandawazi hufanywa na vijana. Lengo kuu la kutumia maumbo ya lughatandawazi katika Kiswahili ni kufupisha neno fulani na kuokoa muda katika uandishi wa maneno mbalimbali. Hivyo, utumiaji wa lughatandawazi huibua makosa mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti mwingine unaweza kufanywa ili kubaini kama matumizi ya lughatandawazi yanafungamana na kundi la vijana tu au yanaweza kuhusisha makundi mengine ya watumiaji lugha kama vile watoto na wazee.

4.0 Sababu za Makosa ya Kimofolojia Yanayofanywa na Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii imefafanua sababu za makosa ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Makala haya yamebaini sababu mbalimbali zinazosababisha makosa ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji wa Kiswahili (hususani Wahaya) katika mawasiliano yao. Sababu za makosa hayo zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

4.1 Kutokujua vyema Lugha ya Kiswahili

Kutojua ni hali ya kukosa ufahamu au maarifa juu ya jambo au kitu fulani. Hali ya kutojua ruwaza (kanuni na sheria) za lugha husika husababishwa na mtumiaji lugha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kanuni, sheria na taratibu za lugha anayoitumia (Corder, 1974; Ellis, 1997; Jabeen na wenzake, 2015). Makala haya yanadhihirisha kwamba watumiaji wa Kiswahili hufanya makosa ya kimofolojia kwa sababu ya kutoelewa kanuni, sheria na taratibu za lugha ya Kiswahili. Mathalani, watoataarifa vijana na watu wazima waliotoa taarifa za utafiti huu kwa njia ya majadiliano ya vikundi lengwa kuhusu matumizi ya wingi katika maumbo ya maneno mbalimbali, walidai kwamba hawajui ngeli za nomino na hivyo hulazimika maneno mengi kuyapa umbo la wingi (taz. Jedwali Na. 4). Hii ni kwa sababu watumiaji hao hutumia mofu {ma} kurejelea nomino ambazo hazipaswi kuwa na mofu ya wingi. Makosa ya namna hii yamebainishwa na kufafanuliwa bayana katika Kipengele Na. 3.4 kinachohusu makosa ya kutumia ngeli za nomino.

Aidha, watoataarifa hao walipoulizwa kuhusu hali ya umoja na wingi wa maneno walisema kwamba “*maneno mengi katika Kiswahili lazima yawe na umoja na wingi*”. Kutokana na hali hiyo, tunabaini kwamba watu hao hawajui matumizi sahihi ya ngeli za nomino katika Kiswahili, na hivyo huwapa ugumu wa kuzitumia kwa usahihi. Sababu ya kutojua vyema lugha imeshadidiwa katika NUD kwa sababu mwasisi wa nadharia hii anasema kuwa baadhi ya makosa husababishwa na mtumiaji lugha mwenyewe kutojua kanuni za lugha anayoitumia (Corder, 1967). Hali ya kutojua lugha fulani husababisha kuteua maumbo ya maneno yasiyokubalika kwa sababu ya kutokuwa sahihi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, baadhi ya maneno ya Kiswahili yanapotumiwa bila kujua usahihi wake husababisha makosa na hivyo kubananga lugha ya Kiswahili.

4.2 Athari ya Lugha ya Kwanza katika Kiswahili

L1 ni ile ambayo mtu huipata au kuiamili kutoka kwa wazazi, walezi au jamii inayomzunguka, ambapo mtu huendelea kuitumia katika maisha yake yote (Stern, 1983). Data za makala haya zinadhihirisha kwamba lugha ya Kihaya ina athari kubwa katika lugha ya Kiswahili. Athari hizo hutokana na uhawilishaji wa maumbo ya maneno ya Kihaya katika Kiswahili. Mathalani, baadhi ya maneno ya Kihaya huishia na viambishi {yo} na {mu} ambavyo huhawilishwa kuwa kiambishi {po} na {mo} mtawalia katika Kiswahili, hivyo, kuzua makosa kama ilivyobainishwa katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6: Mifano ya Maneno ya Kihaya Yanayohawilishwa na Kutumiwa katika Kiswahili

Na.	Neno la Kihaya	Kosa katika Kiswahili	Maneno Sahihi ya Kiswahili
i.	<i>ndaijayo</i>	<i>nitakujapo</i>	nitakuja huko
ii.	<i>walugayo</i>	<i>umetokapo</i>	umetoka huko
iii.	<i>nashubamu</i>	<i>nimerudimo</i>	nimerudi humu
iv.	<i>tekamu</i>	<i>wekamo</i>	weka humu

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Mifano ya maneno katika Jedwali Na. 6 inaonesha mofu za Kihaya ambazo huhawilishwa na kutumiwa katika Kiswahili. Utumiaji wa maneno hayo hutokana na athari ya lugha ya Kihaya katika kutumia lugha ya Kiswahili. Sababu ya athari ya L1 katika kutumia Kiswahili inashadidiwa vyema katika NUD kwa sababu makosa mengi katika lugha husababishwa na mwingiliano wa L1 na L2 (Corder, 1967). Aidha, athari za L1 husababisha uhamishaji wa ruwaza za L1 katika utumiaji wa L2 ambapo viambishi vya lugha moja hutumiwa katika lugha nyingine. Hivyo basi, kutokana na athari hizo, baadhi ya Wahaya huamini kwamba kanuni za lugha ya Kiswahili na Kihaya zinafanana katika lugha zote mbili, jambo ambalo si sahihi.

Aidha, athari ya lugha ya kwanza katika Kiswahili husababisha kutumia tafsiri sisisi katika maneno ya Kiswahili. Tafsiri sisisi ni mbinu ya tafsiri ambapo maneno hutafsiriwa kwa kuzingatia maana zake za msingi katika lugha chanzi kwa kufuata sarufi ya lugha lengwa bila kuzingatia utamaduni wa lugha lengwa (Newmark, 1988). Data ya makala haya imebaini makosa mbalimbali ya kutumia maneno kutokana na tafsiri sisisi kama yanavyobainishwa katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 7: Mifano ya Makosa ya Kutafsiri Sisisi Maneno ya Kihaya

Na.	Neno la Kihaya Lililotafsiriwa	Kosa	Neno/Maneno Sahihi
i.	<i>ningendelao</i>	<i>naendeapo</i>	naendelea vizuri
ii.	<i>ompeo</i>	<i>nipepo</i>	nipe
iii.	<i>otabingambila</i>	<i>usiviniambie</i>	usiniambie
iv.	<i>olampao</i>	<i>utanipapo</i>	utanipa
v.	<i>tinkubimanya</i>	<i>sivijui</i>	sijui

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Jedwali Na. 7 linaonesha maneno mbalimbali ambayo yametafsiriwa sisisi kutoka lugha ya Kihaya na kutumiwa katika lugha ya Kiswahili. Kutafsiri huko kunaruhusu kuongeza viambishi visivyohitajika kwenye neno. Kwa kurejelea NUD, tunabaini kwamba tafsiri sisisi ni mchakato mmojawapo unaosababisha makosa mbalimbali ya kiisimu yakiwamo ya kimofolojia. Hii ni kwa sababu Corder (1967) anabainisha

wazi kwamba zaidi ya 85% ya makosa, hutokana na michakato mbalimbali ya utumiaji lugha ambapo tafsiri ni mchakato mmojawapo. Hivyo basi, kutokana na data hiyo, hatuna budi kusema kwamba tafsiri sisi husababisha makosa kadhaa katika utumiaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili.

4.3 Kutozingatia Matumizi Sahihi ya Msamiati wa Kiswahili

Mtu yeyote anayetumia lugha, anapaswa kufahamu msamiati wa lugha husika ambao ni sahihi na unaoendana na muktadha wa mawasiliano. Hali ya kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili usio sahihi, husababishwa na kutozingatia muktadha na wingi-lugha katika jamii; jambo ambalo huibua makosa mbalimbali katika lugha ya Kiswahili (Niyomugabo, 2017). Makala haya yamebaini kwamba makosa ya kimofolojia husababisha kutumia msamiati wa Kiswahili usio sahihi. Hali hiyo ya kutozingatia matumizi sahihi ya msamiati wa Kiswahili husababisha kutumia maneno ambayo si sahihi katika lugha ya Kiswahili. Data Na. 5 inaonesha majadiliano kutoka kwa watoataarifa vijana ambayo yamenukuliwa kwa maandishi katika dondoo la Data Na. 5.

Data Na. 5

*...kwa kweli maisha ya siku hizi yamekuwa magumu. Pesa azipatikani, ajira hamuna hata kupata **dara** ni shida. Kwa kuwa leo tumekupata wewe utatuacha vizuri... sisi **dara** itatutosha ili tupate **bukubuku**... kuna mutu mmoja alikuja hapa akutuachia chochote... yaani tangia apo **sitakagi kuvisikia vimaneno** vya mtu ambaye ni muongo... sasa wewe unaonekana mstaarabu inabidi **usitufanyie** kama yule jamaa... tukimaliza majadiliano haya kabla ya kukuandikia inabidi utupe dau letu, bila hivyo **hatutavifanya** vingine vya kuandika.... **ukifeli** hapo itabidi utafute wadau wengine wa kukuandikia....*

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Maneno yaliyopigiwa mstari katika Data Na. 5 yamechambuliwa na kubainishwa katika Jedwali Na. 8 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 8: Mifano ya Matumizi ya Msamiati Usio Sahihi

Na.	Neno Lisilo Sahihi	Neno/Maneno Sahihi ya Kiswahili
i.	<i>dala</i>	elfu tano
ii.	<i>bukubuku</i>	elfu mojambo
iii.	<i>sitakagi</i>	sitaki
iv.	<i>kuvisikia</i>	kusikia
v.	<i>vimaneno</i>	maneno
vi.	<i>usitufanyie</i>	usifanye
vii.	<i>hatutavifanya</i>	hatutafanya lolote
viii.	<i>ukifeli*</i>	ukishindwa

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Maneno yaliyopigiwa mstari katika Data Na. 5 na kubainishwa katika Jedwali Na. 8 yanaonesha matumizi ya msamiati usio sahihi ambao unatokana na kutumia tafsiri sisizi kutoka lugha ya Kihaya na lugha nyinginezo na kutumiwa katika lugha ya Kiswahili. Sababu hii inashadidiwa katika NUD kwani zaidi ya 85% ya sababu za makosa hujitokeza katika mchakato wa kutumia lugha husika ambapo tafsiri ni mchakato mmojawapo wa kutumia lugha. Hata hivyo, makala haya yanaonesha kuwa tafsiri sisizi siyo mchakato pekee unaosababisha makosa, bali ipo michakato mingine inayosababisha makosa katika kutumia lugha ya Kiswahili.

Aidha, makala haya yanadhihirisha kwamba maneno yanayotafsiriwa sisizi hayatokani na lugha za Kibantu pekee, bali kuna maneno mengine hutoka katika lugha za kigeni yanayotokana na uchanganyaji msimbo na kutumiwa katika Kiswahili. Kwa mfano, neno *ukifeli* limetokana na uchanganyaji msimbo yaani {uki + fail} na kuunda neno 'ukifeli', japo neno hilo ni sanifu katika lugha ya Kiswahili. Vilevile, mtafiti amebaini kwamba baadhi ya maneno kama vile *dala* na *bukubuku* hayatokani na tafsiri sisizi wala uchanganyaji msimbo, bali yanatokana na ujumuishaji. Mathalani, watoataarifa walipoulizwa maana ya maneno hayo na usahihi wake katika lugha ya Kiswahili walisema, “Sisi tunajua maneno hayo ni sahihi kwa kuwa watu wengi wanayatumia wanapozungumza Kiswahili... na hivyo ni vigumu kujua yametokana na nini.” Kutokana na hali hiyo, tunabaini kwamba matumizi ya msamiati sahihi yasipozingatiwa husababisha mtumiaji lugha kutopata umilisi wa lugha husika. Kwa mantiki hiyo, mtumiaji wa Kiswahili anapaswa kutumia maneno sahihi na yanayokubalika katika lugha hiyo.

4.4 Ufanano wa Maneno ya Lugha za Kiswahili na Kihaya

Ufanano ni hali ya kulandana kwa umbo na sura. Ufanano huo unaweza kuwa wa kisauti, kiumbo, kimuundo au kimaana. Kimofolojia, ufanano wa maneno ni hali ya neno fulani katika lugha moja kufananishwa na neno jingine katika lugha nyingine. Kiswahili na Kihaya ni lugha za Kibantu zenye kufanana na kutofautiana katika vipengele mbalimbali vya kiisimu. Makala haya yanadhihirisha maumbo ya maneno ya Kiswahili ambayo yanafanana na maneno ya Kihaya kiumbo na kimaana, licha ya kwamba baadhi ya maneno yameongezwa viambishi tangulizi na mengine kupachikwa sauti katikati mwa neno husika. Maneno hayo ambayo yalidondolewa katika majadiliano ya vikundi lengwa yamebainishwa katika Jedwali Na.9 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 9: Mifano ya Maneno ya Kihaya Yanayofanana na Maneno ya Kiswahili

Na.	Neno la Kihaya	Neno la Kiswahili
i.	<i>bona</i>	ona
ii.	<i>enyanya</i>	nyanya
iii.	<i>ekitunguru</i>	kitunguu
iv.	<i>ensenene</i>	senene
v.	<i>loga</i>	loga

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Mifano ya maneno iliyotolewa katika Jedwali Na. 9 hapo juu inaonesha uongezaji wa kiambishi tangulizi {e+nyanya}, kiambishi tangulizi na sauti nyingine {e+n+senene, e+kitungu+r+u}, uongezaji wa sauti tu {b+ona} na kutoongeza sauti yoyote wala kiambishi tangulizi chochote {loga}. Kutokana na ufanano wa maneno hayo kiumbo, imebainika kwamba hata maana ya maneno hayo inafanana katika lugha zote mbili. Hata hivyo, makala haya hayakuchunguza sababu za ufanano wa maumbo hayo katika lugha ya Kihaya na Kiswahili kwa kuwa halikuwa lengo la makala haya, bali makala haya yamechunguza maumbo ya maneno hayo na maana zake katika lugha hizo mbili. Hivyo, kwa kurejelea NUD tunabaini kwamba mwingiliano wa L1 na L2 husababisha watumiaji wa lugha kufanya makosa ya namna hiyo wanapotumia lugha husika (Corder, 1967). Kwa mantiki hiyo, ufanano wa baadhi ya maneno ya Kiswahili na Kihaya husababishwa na mwingiliano uliopo baina ya watu katika utumiaji wa Kiswahili na hivyo kuibua makosa kadha wa kadha.

Aidha, katika Jedwali Na. 9 tunabaini uongezaji wa kiambishi tangulizi {e} katika baadhi ya maneno. Hata hivyo, uongezaji wa kiambishi tangulizi hauathiri maana ya msingi ya neno husika katika lugha ya Kihaya. Hali hii ni kawaida katika lugha za Kibantu, kwani nomino za Kihaya hukubali kuambikwa viambishi tangulizi {a, e na o} ambavyo haviathiri maana ya neno (Buberwa, 2014). Hivyo basi, baadhi ya maneno ya Kihaya yanapotumiwa katika Kiswahili huibua makosa mbalimbali kwa sababu ya kuruhusu kuongeza maumbo mengine yasiyokubalika katika lugha ya Kiswahili.

5.0 Hitimisho

Makala haya yamechambua makosa anuwai ya kimofolojia yanayofanywa na watumiaji lugha ya Kiswahili hususani Wahaya na sababu za makosa hayo. Kutumia maumbo ya maneno ya lugha ya Kiswahili yenye makosa husababisha athari kadhaa katika lugha ya Kiswahili. Mathalani, neno lolote lisipoeleweka vyema huzua utata na hivyo kutanza mawasiliano. Pia, mtumiaji yeyote wa lugha anapozoea kutumia maneno yasiyo sahihi hushindwa kumudu ruwaza za lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, watumiaji wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine

hawana budi kuacha ujumuishaji wa kuhawilisha maumbo yasiyo sahihi na kujifunza ngeli za nomino ili waweze kutumia maumbo sahihi ambayo yanakubalika katika lugha ya Kiswahili ili kuzingatia sarufi ya lugha ya Kiswahili, utamaduni wa jamii na kuepuka kubananga lugha ya Kiswahili.

Marejeleo

- Buberwa, A. (2014) "Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika". *Kiswahili*, Juz. Na. 77: 41-61.
- Champungu, S. I. (2019) *Muundo na Dhima za Vibainishi Vioneshi katika Kiswahili Sanifu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Corder, S. P. (1967) "The Significance of Learner's Errors". *International Review of Applied Linguistics*, Juz. Na. 5: 161-170.
- Corder, S. P. (1974) *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. London: Longman.
- Ellis, R. (1997) *The study of Second Language Acquisition*. Oxford: OUP.
- Hepkwony, L. C. (2011) *Matatizo ya Kisarufi Miongoni mwa Wanafunzi wa Kikipsigis Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Lugha Kadirifu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Hussein, H. A. (2016) *Mabadiliko ya Kifonolojia na Kisemantiki katika Maneno ya Kiswahili yenye Asili ya Kiarabu*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.
- Jabeen, A., Kazemian, B. na Mustafai, M. S. (2015) "The Role of Error Analysis in Teaching and Learning of Second and Foreign Language". *Education and Linguistics Research*, Juz. 1(2): 52-60.
- Joster, F. N. (2018) "Makosa ya Kiuhariri katika Vitabu vya Kiada vya Kiswahili nchini Tanzania". Katika S. Omari na M. Samwel (Wah.) *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika: Kwa Heshima ya Prof. M.M. Mulokozi*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 419-441.
- Kemunto, A. B., Ernest, M. S. na Omari, O. J. (2017) "Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili ya Wanafunzi wa Shule za Upili Nchini Kenya". *International Journal of Arts and Education*, Juz. Na. 1(2): 13-24.
- Kihore, Y.M., Massamba, D.B.P. na Msanjila, Y.P. (2007) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kiparsky, P. (1982) *Lexical Morphology and Phonology: Linguistics in the Morning Calm*. Seoul: Hanshin Publishing Co.
- Kisakwah, B.A. (2014) *Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba*. Tasnifu ya Umahiri (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.
- Larsen, D. (1992) *An Introduction to Second Language Acquisitions Research*. London: Longman.

- Leonard, G. (2008) *Morphological Marking for Syntactic Relations in Ruhaya*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Mghase, G. E. (2011) *Makosa ya Kiisimu katika Uandishi wa Magazeti*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Mohammed, N.A. (2013) *Matumizi ya Lughatandawazi katika Simu za Kiganjani: Changamoto katika Lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Mpemba, T. (2018) “Matatizo ya Uandishi katika Kiswahili: Maana, Chanzo na Ufumbuzi”. Katika S. Omari na M. Samwel (Wah.) *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika: Kwa Heshima ya Prof. M.M. Mulokozi*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 442-474.
- Mugaya, T. S. (2018) *Mofolojia Changamani ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.
- Mutembei, A. (2011) Kukitandawazisha Kiswahili Kupitia Simu za Kiganjani: Tafakari kuhusu Isimujamii. *Swahili Forum*, Juz. 18: 198-210.
- Mutugu, B.N. (2001) *Makosa ya Kileksia katika Insha na Chanzo Chake: Uchunguzi wa Shule Tano na Upili Wilayani Kiambu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Muysken, P. (2000) *Bilingual Speech: A Typology of Code-Mixing*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Newmark, P. (1988) *A Textbook of Translation*. London: Prentice Hall.
- Niyomugabo, C. (2017) “Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Rwanda: Historia, Tathmini ya Makosa, matatizo na mahitaji”. *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 79: 78-92.
- Nyagah, S. K. (2016) *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia Yanayojitokeza katika Kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Upili Tigania Jimbo la Meru*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.
- Obara, J. M. (2014) *Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.
- Rapando, M. (2005) *Makosa ya Kimofolojia-sintaksia katika Kazi za Kiswahili zilizoandikwa na Wanafunzi wa shule za Upili jijini Nairobi*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.
- Stern, H. H. (1983) *Fundamental Concepts of Language Teaching*. Oxford: Oxford University Press.
- TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford: TUKI.